# Mpingo Conservation & Development Initiative

# MCDI Misitu ya Jamii Tanzania
# Umoja wa Uthibitishaji

*SD01 Masharti ya Uanachama*

Swahili – Toleo la 3.2 – 11/20/2013

# Yaliyomo

TAFSIRI YA MANENO ..... 3
SIFA ZA UANACHAMA ..... 4
VIGEZO VYA MSITU ..... 5
KANUNI KUU ..... 10
UVUNAJI USIORUHUSIWA ..... 13
USIMAMIZI WA MOTO ..... 14
VIWANGO VYA WAFANYAKAZI. ..... 16
UVUNAJI WA RASILIMALI ZA MSITU ..... 17
MATISHI YA KUPASULIA MBAO ..... 20
UUZAJI WA MAZAO YA MSITU YALIYOTHIBITISHWA ..... 21
UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU ..... 24

# Tafsiri ya Maneno

**FSC** – Forest Stewardship Council, ni taasisi ya kimataifa ya uthibitishaji.

**Kamati ya Maliasili ya Kijiji** – ni kamati ndogo ya Serikali ya Kijiji yenye majukumu ya kusimamia shughuli zote za maliasili katika Kijiji.

**Kijiji** – ni jamii iliyosajiliwa kama kijiji chini ya sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Kila kijiji kina uongozi uliochaguliwa wa **Serikali ya Kijiji**.

**MCDI** – ni Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo ambalo ni asasi isiyo ya kiserikali iliyosajiliwa kisheria, nambari ya usajili 1350.

**Meneja wa Msitu** – ni mtu mmoja au kikundi cha watu wenye mamlaka ya kumiliki na kusimamia misitu ya vijiji.

**Meneja wa Umoja** – ni mtu katika Shirika la kuhifadhi mpingo na maendeleo anayesimamia cheti cha umoja wa Uthibitishaji.

**Msitu wa Jamii** – ni eneo la msitu ndani ya ardhi ya Kijiji (au Vijiji ) lililotengwa kwa madhumuni ya kulisimamia na ambalo lina mpango wa usimamizi uliopitishwa chini ya Sheria ya Misitu ya Tanzania ya mwaka 2002 kama Ardhi ya Msitu wa Hifadhi ya Kijiji.

**Mwongozo wa Urekebishaji** – ni tamko linalotolewa ili kukabiliana au kusahihisha mapungufu katika umoja wa uthibitishaji au katika kanuni na vigezo vya FSC.

# Sifa za Uanachama

**J1.** Uanachama katika Cheti cha Umoja kwa sasa upo wazi kwa Serikali za Vijiji kupitia Kamati za Maliasili za Vijiji ziliyochaguliwa kihalali kulingana na sheria za nchi. Kijiji kinaweza kuomba kuingizwa kwa msitu wa kijiji unaosimamiwa na kamati ya maliasili ya kijiji kwenye mpango wa uthibitishaji.

**J2.** Ili Meneja wa Msitu aweze kujiunga na umoja wa uthibitishaji ni lazima ithibitike kuwa ana uwezo wa kusimamia misitu kulingana na matakwa ya umoja wa uthibitishaji na kanuni na vigezo vya FSC.

**J3.** Isipokuwa katika hali isiyokuwa ya kawaida, na kwa kipindi chote cha uanachama, Meneja wa Misitu lazima aahidi kwamba ataendelea kutunza maeneo yote ya misitu yaliyopo kijijini ambayo wana mamlaka nayo hata kama yapo nje ya eneo la msitu uliothibitishwa.

a) Hili linahusika zaidi kwa kamati za maliasili za vijiji na Kamati za maliasili za muungano wa vijiji katika kusimamia maeneo yaliyopo katika ardhi yao ambayo yamebainishwa kama maeneo ya misitu katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji. Hili pia linawahusu wanavikundi ambao wana jukumu la kusimamia maeneo hayo.

b) Mfano wa hali isiyokuwa ya kawaida inaweza kuwa ni; kwa mfano unahitaji ardhi ya uwekezaji toka nje uliokubaliwa na serikali na endapo mwekezaji yupo tayari kulipa faida kubwa katika kuchukua ardhi.

c) Kulingana na taratibu za cheti cha uthibitishaji, Meneja wa Umoja ataamua kama hali iliyojitokeza inakubalika na mambo gani yazingatiwe.

d) Endapo mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji utabadilishwa kupunguza eneo la msitu, jambo hili ni lazima lipitishwe na mkutano mkuu wa kijiji. Nakala ya muhtasari wa mkutano pamoja na barua inayoeleza sababu za mabadiliko lazima ziwasilishwe kwa Meneja wa Umoja, ambaye atajibu ndani ya kipindi cha mwezi mmoja.

**J4.** Kamati za maliasili za vijiji na kamati za muungano lazima ziwe zimechaguliwa kulingana na sheria za nchi, pamoja na kutimiza sharti la kuwa angalau moja ya tatu ya wajumbe wawe wanawake na angalau mwakilishi mmoja toka kitongoji ambacho kipo karibu zaidi na msitu husika.

**J5.** Mameneja wa misitu lazima wawe wamepata mafunzo ya kutosha juu ya majukumu yao. Shirika la mpingo linatoa mafunzo kwa wanajamii wenye nia ya kusimamia misitu yao. Maelezo kuhusu mafunzo haya yamo katika *ED03 Mwongozo wa Mafunzo ya usimamizi misitu.* Wanajamii waliohudhuria mafunzo mara moja au zaidi huorodheshwa kwenye fomu maalumu-*EF13 Orodha ya Mameneja wa Misitu Waliopewa Mafunzo.* Wale wanaomaliza mafunzo hupewa cheti-*SL09 Cheti cha Kumaliza Mafunzo – Usimamizi wa misitu ya wanajamii.*

a) Angalau nusu ya wanachama wa kamati ya maliasili ya kijiji, muungano wa vijiji au vikundi vya kijamii lazima wawe wamefuzu mafunzo.

b) Angalau mtu mmoja katika kikosi cha doria ya msituni lazima awe amefuzu mafunzo.

**J6.** Mameneja wa misitu lazima waahidi kwamba watakuwa waaminifu katika umoja wa uthibitishaji na kuwa na nia ya kuwa katika chama kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, hata kama hili litalazimu kurekebishwa kwa mpango wa usimamizi misitu. Mameneja wa misitu lazima wafanye kila jitihada kutekeleza masharti yote ya uanachama kwa kipindi chote cha uanachama.

# Vigezo vya Msitu

**J7.** Maeneo yanayosimamiwa kama Misitu ya hifadhi ya vijiji chini ya sheria za nchi ndio pekee yatakayoingizwa katika mpango wa cheti cha pamoja cha uthibitishaji. Kijiji ambacho kina Msitu wa Hifadhi wa Kijiji ni sharti kiwe na Cheti cha Ardhi ya Kijiji au Hati yeyote halali inayotambulika chini ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999.

**J8.** Ili Msitu wa hifadhi ya Kijiji ukubalike ni lazima uwe na sifa zifuatazo;

a) Msitu lazima uwe na uoto mwingi wa miti.

b) Msitu uwe umefunga kivuli si chini ya asilimia ishirini (20%), na urefu wa miti wa wastani wa si chini ya mita 5. Misitu ya matajiwazi (miombo) iliyofunga na isiyofunga yote inaruhusiwa, lakini si uwanda wa nyasi na njenga.

c) Uwe ni uoto wa asili. Umoja wa uthibitishaji hauhusishi misitu ya kupanda.

d) Uoto uwe wa jamii za miti ya asili na sio jamii toka sehemu nyingine.

e) Kusiwepo na uharibifu mkubwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kusiwepo na ukataji miti kwa ajili ya kusafisha mashamba, uchomaji mkaa au matumizi mengine ya misitu.

f) Uvunaji wa magogo kwa kipindi kivupi kilichopita siyo sababu ya kutokukubalika kwa Msitu wa Kijiji. Lakini hii italeta mapato machache kwa kipindi kijacho hadi hapo uoto utakapokuwa tena.

**J9.** Msitu wa Kijiji pia lazima uendane na mpango wa usimamizi misitu. Mpango lazima;

a) Uwe halali chini ya sheria ya Misitu ya Tanzania ya mwaka 2002 pamoja na miongozo mingine ya misitu na uwe umebakiza angalau miaka miwili ya utekelezaji.

b) Uendane sambamba na Kanuni na Vigezo vya FSC. *Kabrasha la SD05 Kanuni kuu na vigezo vya FSC* linabainisha jinsi mameneja wa misitu wanavyotakiwa kutimiza matakwa ya uthibitishaji.

c) Ubainishe kuwa lengo la muda mrefu la kusimamia msitu ni kudumisha uasilia wa msitu.

d) Umetenga angalau 10% ya msitu wa Kijiji kama eneo ambalo uvunaji hautafanyika. Baada ya kutengwa eneo hili halitaweza kubadilishwa isipokuwa kwa sababu maalum pekee, na kwa idhini ya maandishi ya meneja wa umoja.

e) Utazingatia matumizi yote ya desturi na kimila katika msitu kwa vitongoji na vijiji jirani, na hautaathiri haki za wazawa au wakaaji wa eneo hilo au watu waishio pembezoni mwa msitu.

f) Unazuia aina yoyote ya kilimo na ufugaji ndani ya msitu.

g) Unabainisha rasilimali muhimu katika msitu ambazo zinasimamiwa, aina za miti ya mbao na mazao yasiyotimbao (rasilimali zingine).

h) Mipango ya Usimamizi Misitu ambayo ipo katika mfumo wa sasa wa *Mwongozo wa Mpango wa Usimamizi Misitu* itachukuliwa kuwa imetimiza masharti ya vipengele viwili hapo juu.

i) Kamati za maliasili za vijiji, muungano wa vijiji na vikundi vya kijamii ambao ni Mameneja wa Misitu lazima wawe na sheria ndogo zilizopitishwa na mkutano wa kijiji na Halmashauri ya Wilaya (kwa upande wa kamati ya maliasili na muungano wa vijiji) na wanachama wote wa kikundi cha kijamii kwa upande wa vikundi vya kijamii.

**J10.** Ingawa mpango wa usimamizi Msitu wa Hifadhi ndani ya Eneo la Kijiji unaisha baada ya miaka mitano hakuna haja ya kubadilisha eneo la Msitu wa Hifadhi ndani ya Kijiji kwa

matumizi mengineyo hapo baadae. Mpango Shirikishi wa Matumizi bora ya Ardhi ya Kijiji lazima utumike kama uthibitisho kwa hili. Pale ambapo Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi hauonyeshi kwamba ardhi ni kwa ajili ya uhifadhi wa msitu, Meneja wa Misitu lazima amshawishi Meneja wa Umoja wa uthibitishaji kwa maandishi kuwa wana lengo la kusimamia eneo hilo kwa ajili ya uhifadhi wa msitu.

**J11.** Msitu wa kijiji uliothibitishwa ni lazina uwe na mpango wa usimamizi wa moto unaokwenda na wakati kuendana na matakwa ya R29. Mpango wa usimamizi wa moto unaoendana na toleo jipya la *SD09 Mpango wa Usimamizi Moto* utazingatiwa kwa ujumla kama umetimiza matakwa ya kipengele hiki.

**J12.** Kila msitu wa Kijiji uliothibitishwa lazima ubakie katika cheti cha pamoja kwa kipindi cha angalau miaka mitano. Wanachama hawaruhusiwi kubadilisha matumizi ya msitu katika kipindi hicho cha uanachama.

## Kujiunga au kuongeza msitu katika Umoja wa Uthibitishaji

### *Taratibu za kujiunga*

Meneja wa Msitu ambaye ametimiza masharti yote hapo juu anaweza kujiunga kwa kufuata utaratibu ufuatao;

**J13.** Kuwasiliana na Meneja wa Umoja kuonyesha nia ya kujiunga.

**J14.** Mwakilishi wa MCDI atajadiliana na Meneja wa Msitu. Wataangalia kama Meneja wa Msitu na Msitu wenyewe unakidhi masharti ya uthibitishaji. Majadiliano yatahusu;

a) Maelezo ya utambulisho kuhusu Umoja wa Uthibitishaji.

b) Maelezo ya Utambulisho kuhusu FSC. *SD05 Kanuni kuu na vigezo vya FSC* inaweza kutumiwa katika majadiliano haya.

c) Masharti/Kanuni za uanachama.

d) Maelezo mafupi ya namna ya kujiunga, kuongeza msitu na jinsi ya kijitoa uanachama.

e) Maelezo mafupi kuhusu uvunaji, ukaguzi, mwongozo wa urekebishaji, utunzaji kumbukumbu na taratibu za kutoa malalamiko.

**J15.** Baada ya hapo Meneja wa Umoja ataandika barua kuelezea matokeo ya mkutano huo kama ifuatavyo:

a) Kama mwombaji hajakubaliwa, sababu zitatolewa.

b) Kama mwombaji amekubaliwa, tarehe itaonyeshwa katika barua ya lini mwombaji atakuwa mwanachama kamili, pia taratibu zifuazo zitafuata.

**J16.** Jalada litafunguliwa kwa ajili ya mwanachama mtarajiwa. (Barua za kukataliwa pia zitawekwa katika jalada moja.)

**J17.** Meneja wa Umoja atapanga ili mkaguzi wa MCDI amtembelee mwanachama mtarajiwa pamoja na msitu. Wakati wa ukaguzi wa awali, mkaguzi atafanya yafuatayo:

a) Atatoa nakala ya *SD01 Masharti ya Uanachama*, na kuelezea kanuni zote.

b) Kukagua msitu unaokusudiwa kuingizwa katika umoja wa uthibitishaji.

c) Atajaza *Fomu SF01 Ukaguzi wa Awali akiwa na Meneja wa Msitu*.

d) Kujadiliana na meneja wa msitu kuhusu mambo yasiyoendana na masharti ya uanachama na kukubaliana muda wa kuyarekebisha.

e) Kutathimini kama kuna aina yeyote ya miti ya mbao ambayo imevunwa na kupungua kwa kiasi cha 66% kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Kama ipo miti hiyo haitavunwa kwa kipindi cha miaka kumi ijayo kama ilivyobainishwa katika Kanuni ya H1.

f) Kama Mkaguzi wa MCDI atajiridhisha kuwa hamna tatizo lolote la kuzuia kusajiliwa, atamsaidia Meneja wa Msitu kujaza fomu za kujiunga zifuatazo;

   *i. Fomu SF02 Maombi ya Kujiunga*

   *ii. Fomu SF03 Kuongeza Msitu*

g) Mkaguzi anaporudi ofisini atajaza *Fomu EF02 Taarifa ya Ukaguzi wa awali* na ataweka katika jalada taarifa zote zilizokamilika.

h) Baada ya hapo Meneja wa Umoja atafanya yafuatayo:

   i. Kama Meneja wa Msitu amekubalika, ataandikiwa *barua SL01 Taarifa ya Kufaulu Ukaguzi wa Awali.* Barua hii itabainisha kama kuna mapufungu yoyote na muda wa kuyarekebisha.

   ii. Endapo Meneja wa Msitu hajakubaliwa, ataandikiwa *Barua SL02 Taarifa ya kutokufaulu ukaguzi wa awali.* Hii itabainisha mapungu yanayotakiwa kurekebishwa haraka sana na yale ambayo ni ya kawaida ambayo hayaitaji kurekebishwa katika kipindi kifupi kabla Meneja hajasajiliwa.

i) Kama Meneja wa Msitu hajafaulu ukaguzi wa awali. MCDI itarudia zoezi hili mara baada ya mwombaji kutoa taarifa kwa MCDI kuwa tayari mapungu yote yaliyojitokeza katika ukaguzi uliopita yamerekebishwa.

**J18.** Baada ya kupokea fomu *SF02 Maombi ya Kujiunga* na *SF03 Kusajili Msitu,* MCDI itazipitia taarifa zote na kujiridhisha kama mwombaji anastahili kusajiliwa.

**J19.** Kama mambo yote yako sawa, MCDI itampatia Meneja wa Msitu namba ya usajili na namba ya msitu. Pia mwanachma atapatiwa nakala ya *barua SL03 Taarifa ya Kukubaliwa Uananchama* ikielezea kukubalika kwa maombi, nakala ya fomu zilizosainiwa pamoja na nakala ya *SD07 Maelezo kuhusu Malalamiko na taratibu za kukata rufaa*. Uanachama utaanza rasmi baada ya wiki moja toka tarehe ya kuandikwa barua ili kuwepo na muda wa kutosha wa barua kumfikia Mwanachama.

**J20.** Meneja wa Umoja atamwingiza Meneja wa Msitu katika orodha ya Wanachama na Misitu iliyothibitishwa na kulijulisha shirika la uthibitishaji juu ya mwanachama na msitu mpya ndani ya kipindi cha mwezi mmoja.

**J21.** Kama mojawapo ya utaratibu wa kujiunga, wanachama wanatakiwa kukubaliana na kanuni zote kama zilivyobainishwa katika kabrasha hili.

### *Utaratibu wa kuongeza msitu mwingine*

**J22.** Meneja wa Msitu anaweza kuomba kuongeza/kusajiliwa msitu mwingine ambao uko chini ya usimamizi wake, lakini yafuatayo lazima yatekelezwe;

a) Kila msitu lazima ufuzu ukaguzi wa awali kama ilivyobainishwa katika kipengele cha J17 hapo juu.

b) Meneja wa msitu ni lazima ajaze na kusaini *Fomu SF03 Kuongeza Msitu.*

c) MCDI itatoa *Barua SL04 Kukubaliwa kwa Msitu* ikionyesha pia nambari ya usajili ya msitu huo.

d) Msitu utasajiliwa rasmi ndani ya kipindi cha wiki moja ili kutoa muda wa kutosha kwa barua kumfikia Meneja wa Msitu.

e) Meneja wa Umoja atauingiza msitu mpya katika orodha ya wanachama na misitu na kutoa taarifa kwa taasisi ya uthibitishaji juu ya mabadiliko haya.

## Kutoa msitu katika umoja na kuacha uanachama

### *Taratibu za kuutoa msitu*

**J23.** Meneja wa msitu anaweza kuutoa msitu katika umoja wa uthibitishaji wakati wowote ambao anausimamia kwa kutoa taarifa (notisi) ya mwezi mmoja, lakini ni lazima msitu uwe umekuwa katika umoja kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

**J24.** Meneja wa msitu anaweza pia kuutoa msitu endapo ardhi ulipo msitu imebadilishwa na kuwa maeneo ya wazi kwa amri ya Raisi wa nchi kulingana na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 Sehemu ya III.

**J25.** Ili kuutoa msitu Meneja wa Msitu ni lazima ajaze *Fomu SF04 Taarifa ya Kuutoa Msitu Katika Umoja wa Uthibitishaji*, akieleza sababu za kujitoa na kupeleka nakala katika ofisi za MCDI zilizo karibu nae.

**J26.** Notisi au taarifa ya mwezi mmoja itaanza rasmi tarehe ambayo fomu zimepokelewa MCDI. Katika kipindi hiki cha mwezi mmoja, Meneja wa Msitu haruhusiwi kuvuna au kuuza rasilimali za msitu kutoka katika msitu unaotarajiwa kutolewa.

**J27.** MCDI itafuta namba ya usajili ya mwanachama siku ambayo notisi/taarifa ya kujitoa imekwisha na mwanachama atapewa taarifa. Meneja wa uthibitishaji atarekebisha orodha ya wanachama na misitu na kuitaarifu taasisi ya uthibitishaji juu ya mabadiliko hayo mara moja.

**J28.** Endapo Meneja wa Msitu atataka tena kuusajili Msitu ambao alishautoa katika umoja wa uthibitishaji, itamlazimu kufuata taratibu zote za kusajili msitu kama ilivyoelezwa hapo juu, na msitu utapewa nambari mpya ya usajili.

**J29.** Isipokuwa kama mwanachama ametolewa katika Umoja kwa kushindwa kutimiza masharti ya uanachama kama ambavyo imeelezwa katika kipengele cha kutolewa uanachama hapo, Mameneja wa Misitu wanaweza kuitoa misitu yao katika umoja wakati wowote ili mradi tu watatoa notisi ya mwezi mmoja na wawe wamekuwepo katika umoja kwa kipindi cha miaka mitano. Mameneja wa misitu wanaotaka kufanya hivyo ni lazima wajaze *Fomu SF05 Taarifa ya Kujitoa Katika Umoja*, wakielezea sababu za kujitoa na kupeleka nakala iliyosainiwa kwa ofisi ya MCDI iliyokaribu.

**J30.** Notisi ya mwezi mmoja inaanza tu siku ambayo fomu zilizosainiwa zimepokelewa katika ofisi ya MCDI. Meneja wa Msitu haruhusiwi kuvuna au kuuza mazao ya misitu toka msitu uliothibitishwa kwa kipindi hicho cha notisi (mwezi mmoja).

**J31.** MCDI itafuta namba ya usajili ya mwanachama siku ambayo notisi/taarifa ya kujitoa imekwisha na mwanachama atapewa taarifa. Meneja wa uthibitishaji atarekebisha orodha ya wanachama na misitu na kuitaarifu taasisi ya uthibitishaji juu ya mabadiliko hayo mara moja.

**J32.** Wanachama ambao walijitoa kwa hiari yao, wanaruhusiwa kujiunga tena kama wataonyesha kuwa usimamizi wa msitu wao umeendelea kufuata taratibu za uthibitishaji kwa kipindi ambacho hawakuwa wanachama.

### *Kutolewa katika Umoja wa uthibitishaji Misitu*

**J33.** Kutolewa katika Umopja ni hatua ya mwisho ya kufukuzwa kwa wanachama ambao hawafuati masharti ya uanachama. Wanachama watavuliwa uanachama endapo:

a) Watazuia watalaam wa MCDI, taasisi ya uthibitishaji na wawakilishi wa FSC kutembelea msitu kwa ajili ukaguzi.

b) Watashindwa kurekebisha mapungufu katika kipindi kilichokubalika.

c) Kutumia vibaya nembo ya Umoja au nembo ya FSC.

d) Kuvunjika kwa kikundi, kama mwanachama ni kikundi cha kijamii au mtandao wa kijamii.

**J34.** Endapo mojawapo ya mambo yaliyotajwa hapo juu yamefanywa, MCDI itachukua hatua zifuatazo:

a) Kama mwanachama ameshindwa kurekebisha mapungu katika kipindi kilichokubaliwa kama ilivyobainishwa katika taratibu za Mwongo wa urekebishaji, hatua za kuvuliwa uanachama zitafuatwa.

b) Meneja wa Umoja atamtumia mwanachama *barua SL05 Taarifa ya Kutaka Kutolewa Uanachama* ikielezea sababu za kutaka kuvuliwa uanachama na taratibu zitakazofuatwa.

c) Wakati taratibu za kutolewa uanachama zikianza, mwanachama haruhusiwi kuziita rasilimali za misitu anazouza au kuzitafutia soko kuwa zimethibitishwa au kusema msitu anaousimamia umethibitishwa.

d) Mwanachama ana haki ya kukata rufaa ndani ya kipindi cha siku 30.

e) Kama rufaa haikupokelewa ndani ya kipindi cha siku 30 basi mwanachama atakuwa ameshatolewa katika umoja.

f) Kama mwanachama atakata rufaa, taratibu za rufaa zitafuatwa kama ilivyobainishwa katika *SD08 Utaratibu wa Kutoa Malalamiko na Kukata Rufaa*.

g) Mara mwanachama anapoondolewa, Meneja wa Umoja atarekebisha taarifa za wanachama na misitu katika orodha yake na kuitaarifu taasisi ya uthibitishaji haraka iwezekanavyo.

**J35.** Wanachama ambao walitolewa katika umoja, hawataruhusiwa kujiunga tena ndani ya kipindi cha angalau miaka mitano.

# Kanuni Kuu

**R1.** Wanachama wanatakiwa kuendelea kusimamia misitu iliyo chini ya Cheti Cha pamoja kulingana na matakwa na vigezo vya FSC. Kabrasha la *SD05 Kanuni Kuu na Vigezo vya FSC*, limebainisha kinachotakiwa kufanywa na mameneja wa Misitu.

**R2.** Wanachama wote ni sharti wafuate sheria zote za nchi, taratibu na miongozo ya Halmashauri ya Wilaya.

**R3.** Usimamizi wa Msitu wa Jamii ni sharti uzingatie kutokuleta mabadiliko na athari katika hali ya uasilia ya msitu.

**R4.** Shughuli zifuatazo hazitaruhusiwa msituni;

a) Ukataji wa miti kwa sababu yeyote ile, isipokuwa kama inahusiana na ujenzi wa barabara kama ilivyobainishwa hapo chini.

b) Malisho ya mifugo.

c) Matumizi ya madawa ya kemikali.

d) Matumizi ya njia za kibaolojia katika shughuli za misitu bila idhini ya Meneja wa Umoja.

e) Matumizi ya mimea iliyokuzwa kwa njia za kibaolojia.

f) Ukuzaji wa jamii za miti zisizo za asili isipokuwa kwa zile zinazopatikana katika misitu ya miombo.

g) Kuendesha magari pembezoni mwa vyanzo vya maji

h) Kuhifadhi au kutupa mafuta yanayoweza kushika moto

i) Kutupa takataka au uchafu

**R5.** Shughuli zozote ambazo zinaweza kuathiri eneo la msitu kwa mfano, ujenzi wa barabara kupitia msituni zitaruhusiwa tu endapo kutakuwa na mahitaji ya Halmashauri ya Wilaya. Kinyume na hili ni lazima maombi ya maandishi yatumwe kwa meneja wa umoja ili ifanyike tathmini ya athari za mazingira kwa barabara iliyopendekezwa, na fomu *SF09 Tathimini ya Ujenzi wa Barabara kwenye Mazingira* itatumika. Thathmini hii itafanyika ndani ya miezi mitatu baada ya maombi kupokelewa, na gharama zote za tathmini lazima zilipwe na mwanachama isipokuwa kama imefutwa na meneja wa umoja. Kama pendekezo litaruhusiwa ukataji miti katika eneo la msitu lazima uwe wa wastani na ujenzi wa barabara uzingatie kupunguza adhari za kimazingira.

**R6.** Wanachama pia wanawajibika;

a) Kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazofanywa na waajiriwa au watu walioingia nao mkataba zinatimiza masharti ya Umoja wa Uthibitishaji, Kanuni na vigezo vya FSC pamoja na sheria za Tanzania, taratibu za Halmashauri ya Wilaya na sheria ndogo za vijiji.

b) Kufuata mpango wa usimamizi misitu uliowakilishwa katika kusajili msitu wa jamii chini ya mpango wa Umoja wa Uthibitishaji (Cheti Cha Umoja).

c) Kutunza kumbukumbu zote, pia kumbukumbu hizo ni lazima ziendane na wakati kama ilivyoonyeshwa hapo chini.

d) Kutekeleza mpango wa urekebishaji kulingana na muda uliokubalika.

**R7.** Ukaguzi kwa kila mwanachama utafanyika angalau mara moja kwa mwaka kama ilivyoainishwa hapa chini. Wanachama wote watafanyiwa tathmini ya mwaka na kurekebisha mapungufu yote yaliyojitokeza. Wanachama wanaweza kutembelewa na mkaguzi wa mahesabu wa umoja wakati wa tathmini ya mwaka, pia na wadau wengine. Wanachama wanapaswa kutoa ushirikiano wao kwa wakaguzi wote wa ndani na nje.

**R8.** Wanachama wanaridhia kwa Meneja wa Umoja kuweka wazi mpango wa usimamizi Msitu, Mpango wa uvunaji na Mpango kazi wa misitu ya jamii iliyothibitishwa na kuwapa nakala wadau wanaohitaji.

**R9.** Wanachama lazima watatue migogoro iliyopo kwa taratibu zilizokubalika. Mgogoro wa ardhi ambao utahusisha msitu uliothibitishwa lazima utatuliwe kulingana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya vijiji ya mwaka 1999. Migogoro ndani ya kijiji ni lazima ifuate taratibu za serikali za kutatua migogoro. Uvunaji hauruhisiwi kufanyika katika misitu yenye migogoro katika kipindi cha utatuzi wa migogoro.

**R10.** Eneo lote la mpaka unaozunguka msitu wa jamii lazima uwekewe alama ya mstari uliopakwa rangi katika kimo cha kifua (mita 1.3) kuzunguka shina la kila mti ulioko kwenye mpaka, Rangi zilizopendekezwa kupakwa ni kama ifuatavyo, ingawa si muhimu sana;

*a)* Mipaka ya nje ya msitu *(Bluu)*

*b)* Eneo la msitu liliotengwa ambalo halitavunwa kabisa *(Njano)*

*c)* Maeneo mengine ambayo yanaonekana sio salama kwa uvunaji kulingana na kanuni ya H5 *(Nyekundu)*

d) Mipaka ya Msitu na mipaka ya eneo lisilovunwa lazima iwekwe alama katika hatua ya mwanzo ya kutenga msitu na alama zitunzwe na meneja wa msitu. Maeneo mengine yatakayobainika hayafai kwa kuvuna yatengwe wakati wowote ikihitajika wakati wa uvunaji.

**R11.** Kama mpango wa usimamizi utarekebishwa (muda wa utekelezaji ni miaka mitano), lazima uwakilishwe kwa Afisa Misitu wa Wilaya na MCDI ili upitishwe.

a) Mipango ambayo iliandaliwa kufuata mwongozo wa uandaaji mpango wa usimamizi misitu itakubalika.

b) Meneja wa Umoja atapitisha au kutopitisha mipango iliyowasilishwa baada ya kuifanyia tathmini katika kipindi cha mwezi mmoja na kuwaajulisha Mameneja wa Misitu juu ya uamuzi wake.

c) Kama mpango wa usimamizi hautaendana na matakwa yanayotakiwa, Meneja wa umoja atatoa mwongozo wa urekebishaji haraka iwezekanavyo.

d) Kama kuna mambo yasiokubaliana na mpango wa usimamizi, Meneja wa Umoja atatoa maelekezo ya kushughulikia mambo hayo.

**R12.** Wanachama wa umoja wanatakiwa kuandaa mpango wa kazi wa mwaka na bajeti ya mwaka kwa kila msitu wa wanaousimamia na kuwasilisha nakala kwa meneja wa umoja. Fomu *SF13 Mpango Kazi wa Mwaka na Bajeti* unaweza kutumika, lakini utaratibu mwigine pia unakubalika. Kwa kawaida bajeti na mpango kazi ni lazima zifuatwe mwaka wa fedha. Bajeti ionyeshe mapato tarajiwa ukiondolea kodi mara utaratibu wa kulipa kodi ya mapato utakapokamilika.

**R13.** Kila mwisho wa mwaka, pamoja na kuandaa bajeti na mpango kazi wa mwaka unaofuata, kila mwanachama anatakiwa aandae ripoti ya mwaka uliokwisha ikijumuisha taarifa ya mapato na matumizi ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliokwisha. Fomu *SF22 Ripoti ya Mwaka ya Meneja wa Msitu* itatumika kwa kazi hii, ila mpangilio mwingine unaruhusiwa.

**R14.** Katika Usimamizi wa msitu, wanachama wanatakiwa kutumia 50% ya mapato yatokanayo na msitu kwa ajili ya gharama za usimamizi kama vile doria na kuzuia moto.

a) Kama wanachama watakuwa hawajaanza kupata mapato ya kutosha toka msituni wanaweza wakasamehewa kutumiza sharti hili kulingana na uamuzi wa Meneja wa Umoja.

b) Meneja wa Umoja atawaandikia wanachama barua *SL08 Taarifa za Msamaha wa Shughuli za Usimamizi Misitu*.

c) Taratibu za MCDI za malipo kwa jamii vitatumika wakati wa kulipa wanajamii watakaofanya kazi msituni.

**R15.** Endapo wajumbe wa Kamati za maliasili za vijiji, kamati za maliasili za muungano au vikundi vya kijamii watabadilishwa mameneja wa misitu wanatakiwa kutoa taarifa kwa Meneja wa Umoja haraka iwezekanavyo, kwa kuwasilisha majina ya wajumbe walioondoka na wale wapya. Iwapo idadi ya wajumbe waliopewa mafunzo itapungua chini ya idadi inayoonyeshwa kwenye kipengele cha J5, idadi ya kutosha ya wajumbe lazima wapatiwe mafunzo haraka iwezekanavyo. Endapo Mameneja wa misitu wana fedha za kutosha gharama za mafunzo haya ya ziada zitakuwa juu yao.

**R16.** Wanachama wanapaswa kuweka kumbukumbu za mahesabu ya misitu yao iliyothibitishwa vizuri na ziwe sahihi na zinazoendana na wakati na zitenganishwe na kumbukumbu za shughuli zingine; kimsingi mahesabu ya kamati ya maliasili ni lazima yatenganishwe na ya serikali ya kijiji.

**R17.** Wanachama lazima watoe taarifa kwa meneja wa umoja haraka iwezekanavyo kama kuna jambo lolote jipya la muhimu linalohusiana na uanachama wao au kama kuna msitu mpya ambao uko chini ya usimamizi wao unahitaji kuingizwa katika cheti cha Umoja.

**R18.** Mwanachama yeyote anaweza kuomba kubadilishwa kwa kanuni moja au zaidi za uanachama au taratibu zozote kwa kumwandikia meneja wa umoja. Meneja wa umoja atajibu kwa barua ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na kutoa maelezo kama ifuatavyo:

a) Ombi sio la msingi na halitaweza kuzingatiwa zaidi.

b) Ombi ni la msingi na litazingatiwa kwenye mchakato ujao wa mwaka wa kuziangalia upya kanuni.

c) Ombi ni la msingi na la haraka sana, na kwamba litafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo.

# Uvunaji Usioruhusiwa

**R19.** Wanachama ni lazima wahakikishe kuwa hakuna uvunaji haramu unafanyika katika msitu wa jamii uliothibitishwa ambao uko chini ya usimamizi wao. Hii ni pamoja na:

a) Kamati za Maliasili za Kijiji kutengeneza sheria ndogo za kusimamia msitu.

b) Doria za mara kwa mara msituni kubaini uvunaji haramu na kuwakamata wahalifu.

i. Doria ifanyike angalau mara mbili kwa mwezi na mara nyingi zaidi ikiwa msitu unaweza kuingilika bila watu kujua, kwa mfano kama kuna njia za kuingilia msituni ambazo hazipitii kijijini.

ii. Kumbukumbu za doria lazima zitunzwe vizuri na zionekane wakati wa ukaguzi.

iii. Doria ipangwe kwa ratiba ya kushitukiza ili wahalifu wasijue ni lini doria itafanyika. Kikosi cha doria pekee ndio kinatakiwa kujua ni lini doria itafanyike.

c) Watu watakaokamatwa wakivuna bila vibali watashitakiwa kulingana na sheria ndogo na adhabu zao zitawekwa katika kumbukumbu.

**R20.** Endapo mwanachama atabaini uvunaji usioruhusiwa ndani ya Msitu wa Jamii uliothibitishwa ambao upo chini ya usimamizi wake ni lazima atoe taarifa MCDI haraka iwezekanavyo. Mara baada ya kupokea taarifa hizi Meneja wa Umoja au mwakilishi wake atajaza fomu maalum ya *SF12 Matukio ya Uvunaji Haramu* na kuweka kumbukumbu katika jalada la mwanachama. Pia kumbukumbu za uvunaji haramu ni lazima zitunzwe Kijijini.

**R21.** Uvunaji usioruhusiwa kulingana na mpango wa usimamizi utaathiri uendelevu wa kiwango cha uvunaji kama ilivyobainishwa katika mpango wa uvunaji.

a) Uvunaji usioruhusiwa utapunguzwa toka kiwango cha uvunaji isipokuwa kama uvunaji huo uligundulika na taarifa kutolewa MCDI na ikiwa:

i. Jumla ya uvunaji haramu kwa jamii hiyo ya miti kwa kipindi cha mpango wa uvunaji hakizidi 50% ya Kiwango cha Uvunaji.

ii. Kutokana na maoni ya Meneja wa Umoja kama mwanachama amefanya jitihada za kutosha kuzuia uvunaji haramu.

b) Uvunaji haramu ambao haukuripotiwa MCDI lakini ukagundulika wakati wa ziara ya ukaguzi utapunguzwa kutoka katika Kiwango cha Uvunaji.

c) Pale ambapo kiwango cha uvunaji kimemalizika, punguzo lolote itabidi lifanyike katika mpango wa uvunaji unaofuata.

d) Barua ya kutoa taarifa ya kupunguzwa kwa kiwango cha ukataji-*SL07 Taarifa ya Kupunguza Kiasi cha Uvunaji* itatolewa kwa mwanachama.

**R22.** Uvunaji wa mazao ya misitu ambao hauendani na Mpango wa uvunaji, utasababisha kutolewa kwa mwongozo wa urekebishaji isipokuwa tu kama ni kwa kiwango kidogo na kutokana na maoni ya mkaguzi wa MCDI kama ataridhia kuwa uvunaji huo hautaathiri hali ya msitu kwa kiasi kikubwa.

**R23.** Kutokudhibiti uvunaji haramu kwa muda mrefu katika msitu wa jamii uliothibitishwa kutasababisha kutolewa kwa mwongozo wa hali ya juu wa urekebishaji na kufungiwa kuvuna kwa aina hiyo ya miti.

# Usimamizi wa Moto

**R24.** Wanachama lazima waonyeshe nia ya kuchukua tahadhari ili kupunguza matukio ya moto msituni. Inaeleweka kuwa kupambana na matukio ya moto ni gharama na inahitaji nguvu kazi kubwa, hivyo haitegemewi kuwa jitihada kubwa za kupambana na moto zitakuwa zimefanyika kabla ya msitu kuingizwa katika uanachama wa cheti cha pamoja.

**R25.** Ili kuzuia uzalishaji usio wa lazima wa hewa ya ukaa na madhara mengine ya kimazingira, mipaka inayozunguka msitu haita fyekwa. Utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa usafishaji wa mpaka wa msitu kwa njia ya ufyekaji una madhara makubwa ukilinganisha na zoezi la ubabuaji haswa katika suala la uwezo wa msitu kunyonya hewa ya ukaa. Mioto itazuiliwa kwa kutumia mpango madhubuti wa ubabuaji kwa kuzingatia zaidi mipaka ya msitu wa kijiji na hususani kwenye maeneo yanayotambulika zaidi kuwa ndio vyanzo vya mioto au sehemu mioto inapoingilia. Pia ubabuaji utafanyika pembezoni mwa barabara, mapito ya wanyama, njia ndogo za miguu zinazokatiza kwenye msitu wa kijiji, na baadhi ya maeneo ndani ya msitu yatakayochaguliwa kwa mpango maalumu kwa kuzingatia kutokurudia eneo moja kila mwaka.

**R26.** Kila mwaka wanachama watatakiwa kufanya ubabuaji usiopungua upana wa meta 100 ndani ya miezi miwili ya mwisho wa kipindi cha mvua kwenye maeneo yote ya mipaka ya msitu wa kijiji, pande zote za barabara, njia za wanyama na njia ndogo za miguu zinazokatiza kwenye msitu wa kijiji.

**R27.** Kubabua moto ni hatua mojawapo muhimu katika kupambana na moto ili kupunguza majanga ya mioto inayovuka mipaka ya msitu mara kwa mara. Ata hivyo wanachama wataanza shughuli hii baada ya kupata mapato ya mwanzo kutokana na kuuza mazao ya misitu.

a) Kwa mwaka ambao mapato yameanza kupatikana wanachama lazima waanze kubabua moto. Ikiwa hali ya fedha inaruhusu ubabuaji moto ufanywe kwa msitu wote na kwa kufuata taratibu za Idara ya Misitu na nyuki.

b) Kanuni ya R14 itatumika kupata kiwango cha chini cha msitu kitakachobabuliwa.

c) Maeneo ya ndani ya msitu yatakayobabuliwa ni lazima yatofautiane kwa kila mwaka, kila mwaka maeneo tofauti yatababuliwa ili kuzuia kubabua eneo moja kila mwaka na kuzuia kulundikana kwa mboji katika eneo moja.

d) Ubabuaji hautafanyika katika eneo la msitu mnene ambapo hakuna nyasi kavu

**R28.** Wanachama wanategemewa kuchukua tahadhari za kutosha kupambana na moto ndani ya msitu wao na kujitahidi kuzuia uchomaji moto wa makusudi.

**R29.** Ubabuaji ni jambo muhimu linalohitaji umakini kufanyika. Kwa mfano, baada ya kipindi cha mvua maeneo ya msitu hukauka kwa vipindi tofauti hivyo ubabuaji utahitajika kufanyika kwa vipindi tofauti kwa kuzingatia ukaukaji wa maeneo hayo. Kwa sababu hii kila mwanachama atalazimika kuandaa mpango/mwongozo wa uzuiaji moto wa msitu wake. Mpango huu anatakiwa ujumueshe mambo yafuatayo:

a) Ramani ya msitu inayoonyesha maeneo ambayo huathirika na moto zaidi, sehemu moto unapoanzia/unapoingilia na mwelekeo wa usambaaji wa moto. Ramani hii sio lazima iwe ya kitaalamu sana bali iwe inaonyesha maeneo yenye vitu muhimu hususani barabara, mapito ya wanyama na njia ndogo za miguu zinazotumika mara kwa mara ambazo zinakatiza kwenye msitu.

b) Ubabuaji moto wa ziada kwenye maeneo hatari ambayo moto huanzia/huingilia; ubabuaji huu unaweza kufanyika ndani au nje ya msitu wa kijiji.

c) Uainishe maeneo ya msitu yanayokauka kwa haraka zaidi kulinganisha na maeneo mengine ili ubabuaji ufanywe kwenye maeneo tofauti ya msitu kwa kuzingatia muda wa ukaukaji.

Mpango unatakiwa uonyeshe utaratibu wa utekelezaji wa shughuli hii baada ya kipindi cha mvua kuisha, ambapo ubabuaji utafanyika.

d) Uelezee jinsi zoezi hili la ubabuaji moto litakavyosimamiwa ndani ya mipaka ya msitu kama ilivyoainishwa na kanuni R27.

e) Uendane na kanuni na vigezo vya FSC na sheria ya misitu ya Taifa ya mwaka 2002 na miongozo yake.

**R30.** Ramani ya kuonyesha maeneo ya ndani ya msitu yaliyobabuliwa inatakiwa iandaliwe baada ya ubabuaji huo kufanyika ili kuweka kumbukumbu maeneo hayo yasirudiwe kila mwaka kuepusha ukusanyikaji wa mboji. Ramani hii sio lazima iwe ya kitaalamu sana bali iwe pia inaonyesha maeneo yenye vitu muhimu ambavyo vitakuwa kumbukumbu za maeneo hayo yaliyobabuliwa ndani ya msitu. Maeneo yenye vitu muhimu yanaweza kuwa barabara, mapito ya wanyama na njia ndogo za miguu zinazotumika mara kwa mara ambazo zinakatiza kwenye msitu.

**R31.** Ukaguzi wa kushtukiza unaweza kufanyika kukagua kama taratibu za kupambana na moto zinafuatwa.

**R32.** Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa zoezi la ubabuaji, maswala ya usalama na afya yatazingatiwa.

# Viwango vya Wafanyakazi.

**R33.** Mameneja wa misitu hawatakiwi:

a) Kuwatumia kwa nguvu au kuwalazimisha wafanyakazi.

b) Kutoa ajira kwa watoto- hii ni kwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, kiwango cha chini cha ajira Tanzania

c) Kubagua ki jinsia, dini, kisiasa, kabila, uzawa/uraia au rangi ya ngozi katika kuwapata wafanyakazi.

d) Kutumia wafanyakazi wasiokuwa na ujuzi mpaka wapatiwe mafunzo, mfano uvunaji

e) Kutumia wafanyakazi wasiokuwa imara kiafya msituni

**R34.** Mameneja wa misitu lazima waheshimu haki za wanaofanya kazi msituni na kuwashirikisha katika kujadiliana juu ya malipo yao.

**R35.** Mameneja wa misitu wakitoa ajira ya kudumu wataheshimu kiwango cha chini cha mshahara kilichopangwa na serikali ya Tanzania.

**R36.** Mameneja wa misitu watawajibika kufanya jitihada za makusudi na za dhati kujali afya na usalama wa watumishi wao. Hii ni kusema pamoja na kuhakikisha kwamba afya na usalama wa watumishi iko katika hali nzuri kama ambavyo wangependa wao iwe kwa afya na usalama wao.

**R37.** Kanuni zote katika kipengele hiki cha viwango vya wafanyakazi ni kwa ajili ya kazi zote zinazofanyika kijijini na si kwa kazi za msitu tu. Mfano Serikali za vijiji ambazo ni wanachama wa cheti cha pamoja wasitumie nguvu kazi ya watoto wanapokuwa wanajenga shule au barabara.

**R38.** Katika kutafsiri viwango vya wafanyakazi meneja wa umoja anaweza kutoa kiwango kulingana na hali halisi ya eneo husika na kuzingatia hali ya wanajamii wasiojiweza.

**R39.** Watu wote wanaofanya kazi msituni, ikiwa ni pamoja na mameneja wa misitu na wavunaji lazima wawe na:

a) Bima ya afya ya Taifa ya Serikali ya Tanzania

au

b) Bima ya afya ya taasisi zingine binafsi.

**R40.** Athari zozote zitakazotokea katika msitu wa hifadhi kwa mfano mtu kujeruhiwa taarifa lazima itolewe kwa meneja wa umoja ndani ya siku 30 kwa kutumia fomu SF11 *Taarifa ya Majeruhi*. Meneja wa Umoja ataweka kumbukumbu za taarifa zote za majeraha kwenye EF09 *Orodha ya Majeruhi.*

**R41.** Sanduku la huduma ya kwanza lenye vitu vyote muhimu vinavyohitajika kama ilivyo orodheshwa kwenye *SD06 Viwango Salama vya Uvunaji* ni lazima liwepo kijijini muda wote, na liwepo msituni wakati wa shughuli za uvunaji. Sanduku la huduma ya kama ilivyoelezwa kwenye SD06, ni lazima liwepo katika shughuli zote za msituni kama vile doria.

**R42.** Maji safi na salama ya kunywa lazima yatolewe kwa kila mmoja anayefanya kazi ngumu msituni. Wakati wa uvunaji ni jukumu la mnunuzi au meneja wa msitu kuhakikisha hili linatendeka.

**R43.** Tahadhari zichukuliwe kwa watu wanafanya kazi msituni ili wasidhurike na wanyama hatari kama tembo. Pale ambapo watalala porini wakati wa doria ya ndege, wakae sehemu salama na kuwasha moto. Watu waondoke mapema msituni kwa shughuli za mchana kabla ya wanyama hatari hawajaanza kutembea.

# Uvunaji wa Rasilimali za Msitu

**H1.** Wanachama wataruhusu uvunaji wa rasilimali za misitu iliyoko chini ya usimamizi wao kulingana na mpango wa uvunaji uliopitishwa Afisa Misitu wa Wilaya na MCDI.

a) Kila aina ya mti itakuwa na mpango wake wa uvunaji isipokuwa kama imeidhinishwa vinginevyo na Meneja wa Umoja. Idhini hiyo itazingatia kanuni za kiikolojia na itahusisha jamii za miti zinazofanana.

b) Mpango wa uvunaji unaweza kugawanya msitu katika maeneo tofauti ya uvunaji. Uvunaji unaweza kufanyika katika eneo moja au katika msitu mzima kulingana na mapendekezo ya meneja wa msitu.

c) Mpango wa uvunaji ni lazima uzingatie vipimo vya chini vya mzunguko wa miti kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya Misitu ya Tanzania.

d) Mpango wa Uvunaji ni lazima uendane na tathmini shirikishi ya mazao ya misitu iliyofanyika si zaidi ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Tathnini lazima iwe imefuata *Mwongozo wa tathmini na uvunaji endelevu.*

e) Uvunaji hautaruhusiwa kwa aina yoyote ya mti ambao unakadiriwa kuwa umevunwa kwa kiasi kinachozidi 66% katika miaka kumi iliyopita.

f) Mpango wa Uvunaji ni lazima uendane na Kanuni kuu na vigezo vya FSC.

g) Kiwango cha Uvunaji kilichoruhusiwa katika mpango wa uvunaji lazima kiendane na tafsiri ya uendelevu iliyopo katika mwongozo wa tathmini ya rasilimali za misitu na uvunaji endelevu.

h) MCDI inashauri mipango ya uvunaji iendane na mwongozo wa mpango wa uvunaji unaotolewa na shirika ingawa si lazima kufanya hivyo.

i) Meneja wa Umoja atapitisha au kutopitisha mipango ya uvunaji iliyowasilishwa kwake na kuwajulisha mameneja wa misitu kwa maandishi juu ya maamuzi yake ndani ya kipindi cha mwezi mmoja.

**H2.** Ni marufuku kufyeka miti yote kwenye msitu wa hifadhi ya jamii, ila tu uvunaji utafanyika kwa kuchagua aina ya miti iliyoruhusiwa na iliyofikia kiwango cha kuvunwa kwa mujibu wa kanuni zilizopo. (Kuendana na kimo cha chini cha kuvuna kilichobainishwa katika sheria ya misitu).

**H3.** Uvunaji wa miti iliyokufa/iliyokauka hauruhusiwi.

**H4.** Uvunaji utafanyika kipindi cha kiangazi kati ya mwezi wa sita na wa kumi na moja, isipokuwa meneja wa umoja anaweza kuruhusu kwa maandishu uvunaji kufanyika kwa wakati mwingine. Uvunaji hautafanyika katika maeneo ambapo maji yamesimama na udongo una unyevunyevu mwingi. Pia uvunaji hauruhusiwi wakati wa upepo mkali kwani ni hatari.

**H5.** Uvunaji hauruhusiwi katika maeneo yafuatayo;

a) Maeneo yaliyobainishwa kuwa ni hatari katika Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 sehemu ya III. Pia hata kama Waziri wa Ardhi haijatamka kuwa eneo fulani ni hatari, lakini Meneja wa Umoja atabaini kuwa eneo hilo lina vigezo vya kuwa hatari.

b) Kwenye miinuko mikali.

*c)* Eneo lililoko ndani ya mita 60 kutoka katika chanzo cha maji, au kingo za mito ya kudumu, au mito inayotiririsha maji mwaka mzima. Meneja wa Umoja ataweka kumbukumbu ya orodha ya mito yenye sifa hizi kwa kila Wilaya yenye wanachama *(fomu EF10)*

d) Ndani ya mita 20 za chemchem au kingo za vijito vyenye kutiririsha maji mara kwa mara au mita 30 kutoka kwenye kingo ya mto mdogo unaotiririsha maji mara kwa mara. Mpango wa Msitu wa hifadhi ya jamii utabainisha wazi chemchem hizo au vyanzo vya maji.

e) Ndani ya mita 2 sawa na upana wa korongo lililoanzishwa na mkondo wa maji wa mvua za masika.

f) Ndani ya mita 60 ya maeneo yenye umuhimu kimila na kijadi kama ambavyo yameainishwa kwenye mpango wa usimamizi.

g) Ndani ya eneo la asilimia kumi la msitu wa hifadhi ambalo halitavunwa kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni ya J9.d

h) Ndani ya eneo lililovunwa aina moja ya miti kwa kipindi cha miaka 25 iliyopita. Mwanachama ataweka alama ya eneo lililovunwa kwenye ramani ya msitu uliothibitishwa

**H6.** Endapo eneo kubwa la msitu halitakidhi kuvunwa kutokana na kanuni ya R21, hili ni lazima lizingatiwe katika mpango wa uvunaji na kiasi cha kuvuna kitalenga eneo linalohusika tu.

**H7.** Maeneo yote yaliyo karibu na eneo la uvunaji ambayo uvunaji hautafanyika lazima yawekwe alama kulingana na kanuni ya R10 kabla ya kuanza kwa shughuli za uvunaji.

**H8.** Taarifa za uvunaji katika Msitu uliothibitishwa ni lazima zibandikwe katika ubao wa matangazo wa kijiji angalau siku mbili kabla uvunaji haujafanyika. Taarifa au maelezo hayo yaonyeshe;

a) Nani aliyetuma maombi (Jina la kampuni na mwakilishi wake)

b) Lini maombi yalipokelewa, tarehe ya mkutano uliojadili na kupitisha maombi na tarehe ambayo uvunaji unategewa kufanyika

c) Kiasi cha rasilimali zitakazovunwa (makisio ya idadi ya magogo au mita za ujazo)

d) Kipato kinachotarajiwa/Kiasi kilicholipwa

**H9.** Angalau mwakilishi mmoja wa Kamati ya Maliasili ni lazima awepo wakati wa uvunaji ili kuhakikisha kanuni hizi zinafuatwa.

**H10.** Mameneja wa misitu lazima wahakikishe kuwa uvunaji unafanyika kimpangilio kwenye msitu wote wa hifadhi ya jamii. Kila uvunaji kwa mnunuzi mmoja unaweza kufanyika katika eneo moja endapo tu eneo litakalovunwa hautarudiwa kuvunwa kwa aina ile ile ya miti ndani ya kipindi kimoja cha miaka ishirini na tano.

**H11.** Ili kuhakikisha uvunaji endelevu si zaidi ya 50% ya kiwango cha uvunaji wa miti ya daraja moja itavunwa kama ilivyoelezewa kwenye mpango wa uvunaji.

**H12.** Uvunaji katika misitu ya jamii iliyo chini ya cheti cha pamoja cha uthibitishaji lazima ufanyike kwa kuzingatia usalama. Pia ni lazima kupunguza mabaki na kuzuia madhara makubwa kwa mimea iliyokaribu.

a) *SD07 Taratibu za Uvunaji Salama Katika Misitu*, ni Mwongozo utakaotumika kuelezea hatua za kufuata katika uvunaji kwa kuzingatia kanuni za usalama.

b) Angalau ***Msimamizi mmoja wa Uvunaji*** ambaye amefuzu mafunzo na amethibitishwa ni **LAZIMA** awepo kuhakikisha kuwa taratibu za uvunaji zinafuatwa. **Gharama za Msimamizi wa Uvunaji ni juu ya Mteja.**

c) Kama kutakuwa na mteja toka nje mwenye mahitaji maalumu kuhusu ubora, Meneja wa Umoja atahakikisha kuwa msimamizi wa uvunaji anapewa taarifa kuhusu hilo.

d) Msimamizi wa uvunaji atajaza fomu maalumu ya ukaguzi wa uvunaji *SF08 Vigezo vya Uvunaji Salama* na atawasilisha fomu iliyosainiwa kwa Meneja wa Umoja baada ya uvunaji kumalizika.

e) Meneja wa umoja atahakiki shughuli za uvunaji na atatoa mwongozo wa urekebishaji kama kuna mambo ambayo hayakufuatwa.

**H13.** Wanachama hawataruhusu magogo kuondoka msituni kabla magogo na visiki kugongwa nyundo na Afisa Misitu wa Wilaya kama inavyotakiwa na sheria ya Misitu Tanzania. Mnunuzi ndiye atakayelipia gharama za ugongaji nyundo.

**H14.** Aidha, baada ya ukataji, magogo yote lazima yawekwe alama mara moja kwa kutumia muhuri/alama ya Umoja wa Uthibitishaji ili kubainisha kwamba mazao hayo yanatoka katika msitu wa uliothibitishwa. Magogo yote yataandikwa nambari ya mwanachama, nambari ya msitu na tarehe ya uvunaji.

**H15.** Baada ya ukataji, ugongaji nyundo na uwekaji alama, magogo yote lazima yapelekwe haraka katika sehemu ya kuhifadhia iliyopo kijijini.

**H16.** Mabaki ni lazima yapunguzwe katika kila uvunaji kwa njia hizi;

a) Urefu wa kisiki usizidi sentimita 30, isipokuwa kama ni vigumu kulifikia shina.

b) Matawi yote lazima yaondolewe msituni, yauzwe kwa mnunuzi aliyevuna au kwa wateja wengine.

c) Matawi madogo yaliyobaki ni bora yapelekwe kijjini kwa ajili ya kuni kuliko kuachwa msituni

d) Kwa ujumla, mabaki yote msituni yasizidi theluthi ya ujazo wa miti iliyoangushwa.

**H17.** Magogo yaliyovunwa katika msitu uliothibitishwa na ambayo hayajauzwa au kuchukuliwa na mnunuzi yahifadhiwe na yatengwe tofauti na magogo yaliyotoka katika misitu isiyothibitishwa.

**H18.** Wanachama wanatakiwa kuwahimiza wanunuzi kuondoa magogo yao haraka iwezekanavyo. Mwanachama anatakiwa kufanya hivyo kwa kuainisha kwenye mkataba wa kuuziana alioweka na mnunuzi, mfano kumpa mteja miezi mitatu kufanya malipo baada ya hapo magogo yanaweza kuuzwa tena kwa wateja wengine.

**H19.** Wanachama wanaweza kuruhusu uvunaji wa mazao yasiyo timbao kutoka misitu ya jamii iliyothibitishwa ila uvunaji huo ni sharti uendane na mpango wa usimamizi.

**H20.** Wanachama watoe upendeleo kwa wateja wanaotoka maeneo yao ambao wako tayari kulipa bei nzuri ya ushindani ya rasilimali za misitu.

# Matishi ya kupasulia Mbao

**H21.** Magogo yaliyokatwa kipindi cha nyuma yanatakiwa yasafirishwe kutoka msituni yakiwa hayaja pasuliwa hadi eneo la kuhifadhia magogo kijijini ambapo mauzo yatafanyika. Ila kwa wanunuzi wadogowadogo wenye uwezo mdogo wanaweza kuruhusiwa kuchania magogo hayo ndani ya msitu uliothibitishwa endapo meneja wa msitu ataridhia.Mauzo haya yataruhusiwa endapo yafuatayo yatafanyika:

a. Kiasi kinachoruhusiwa kwa ajili ya upasuaji katika matishi kisizidi meta za ujazo ishirini (20$m^3$) kwa wakati mmoja kutoka kwenye msitu huo
b. Mnunuzi anatakiwa awe hajawahi kununua zaidi ya meta za ujazo ishirini (20$m^3$) kwa kipindi cha miezi kumi na mbili iliyopita kutoka kwenye msitu huo.
c. Idadi ya matishi isizidi matatu (3) kwa kila uvunaji kutegemeana na idadi ya miti itakayopasuliwa mbao.

**H22.** Uvunaji huu mdogo wa kuchana mbao ndani ya msitu utafuata sheria zilezile zilizowekwa kwa uvunaji mkubwa. Kwa mfano msimamizi wa uvunaji anatakiwa asimamie zoezi hili ili kuhakisha hatua za kiusalama zinafuatwa, uvunaji usifanyike maeneo ambayo uvunaji wa nyuma ulifanyika, na si miti yote iliyopo katika eneo moja itavunwa, miti itavunwa kwa kuacha mti mmoja baada ya mwingine (si kufyeka yote). Pia kuhakikisha siyo zaidi ya moja ya tatu ya mti utakaobaki msituni kama mabaki/uchafu.

**H23.** Athari za kimazingira lazima zipunguzwe wakati wa uchimaji wa matishi ya kupasulia mbao kama inavyoelezwa hapa chini:

a. Matishi hayaruhusiwi kuchimbwa kwenye eneo la asilimia kumi,kuzunguka vyanzo vya maji na maeneo yenye miteremko mikali.
b. Miti yenye ukubwa wa kuanzia mzunguko wa sentimita kumi (10cm) hairuhusiwi kukatwa/kufyekwa kwa ajili ya kuchimba tishi au wakati wa kubiringisha magogo kuelekea kwenye tishi kwa ajili ya kuchana.
c. Tishi liwe na kina cha kati ya mita moja na nusu hadi mbili (1.5m-2.0m), upana wa kati ya meta moja hadi mbili (1m-2m), na urefu wa tishi utategemeana na urefu wa magogo yatakayochanwa mbao.
d. Tishi lazima lifukiwe vizuri kabisa baada ya kutumia kuepusha majanga kwa binadamu na wanyama

**H24.** Mbao zote zilizopasuliwa lazima zipelekwe kijijini katika eneo maalumu la kuweka magogo kwa ajili ya vipimo na uhakiki kabla ya kupelekwa sehemu nyingine yeyote. Na eneo hili maalumu kwa ajili ya kuweka mazao ya misitu ndilo eneo linalotambilika kwa ajili ya uhakiki wa mwisho wa mazao ya msitu kabla ya kutolewa kijijini.

**H25.** Ili kupunguza ugumu na usumbufu ambao utaathiri uraisi wa kupata uwiano, mnunuzi anatakiwa kununua ujazo wote utakaovunwa na sio mbao zitakazopasuliwa pekee. Mnunuzi anatakiwa kutoa mabaki yenye thamani (mfano mabanzi) nje ya msitu na ni uamuzi wake mwenyewe kuyauza kijijini au mahali pengine popote. Hairuhusiwi kuacha mbao kijijini.

**H26.** Zoezi la upasuaji mbao linatakiwa lizalishe angalau asilimia thelathini (30%) ya mti mzima. Mabaki yasiyoweza kutumika yanatakiwa yawekwe chini kabisa ya tishi kabla halijafukiwa.

**H27.** Meneja wa msitu anatakiwa kujaza fomu SF25 Taarifa za Uchanaji Katika Matishi kwa kila aina ya mti kwenye eneo lililochimbwa tishi. Hii ni kwa ajili ya kumbukumbu za ukaguzi ili kuweza kuimarisha kanuni na taratibu za uthibitishaji.

# Uuzaji wa Mazao ya Msitu yaliyothibitishwa

**S1.** Wanachama wa Umoja wa Uthibitishaji wanaweza kuuza mazao ya msitu kutoka katika msitu uliothibitishwa kwa kupitia Shirika la MCDI au wao wenyewe.

**S2.** Endapo mauzo yatafanyika kwa kupitia shirika la MCDI, kiasi/idadi ya manunuzi, gharama za mauzo, na maelezo mengine ni jukumu la mwanachama kukubaliana na Mteja. Jukumu la MCDI ni kusimamia/kuwezesha zoezi hilo kama mwakilishi wa mwanachama. Hivyo basi ni jukumu la mwanachama kuhakikisha mauzo yote yamekamilika na pia maelezo yote ya kimaandishi yako katika mpangilio sahihi.

**S3.** Wanachama wa Umoja wa Uthibitishaji wanatakiwa kuuza mazao yaliyothibitishwa katika eneo lililotengwa ndani ya ardhi ya kijiji, na ni jukumu la mnunuzi kutoa mazao hayo ndani ya eneo hilo.

**S4.** Wanachama wa Umoja wa Uthibitishaji wanaouza mazao ya msitu yaliyothibitishwa wanatakiwa kuweka bayana kwa mnunuzi yafuatayo:

a) Chanzo cha mazao ya Msitu

b) Kiwango cha uthibitishaji kama FSC halisi (100% FSC)

c) Jina la cheti cha Umoja wa uthibitishaji (Shirika la kuhifadhi Mpingo na Maendeleo) na Namba ya Usajili (SA-FM/COC-002151)

d) Jina na namba ya uanachama wa umoja.

**S5.** Sheria hizi za manunuzi ya mazao ya msitu yaliyothibitishwa zitahusika kwa wanunuzi wote walioko kwenye mlolongo wa kuthibitishwa na kujulikana na FSC na wale ambao hawapo kwenye mlolongo wa uthibitishwaji pia.

**S6.** Taratibu zifuatazo lazima zifuatwe wakati wa kufanya mauzo.

a) Awali, mnunuzi atawasilisha maombi ya manunuzi ya mazao ya msitu kijijini kwa maandishi. Kwa makampuni makubwa maombi yao yatawasilishwa kijijini kama Oda ya manunuzi, wanunuzi wengine watatuma barua ya maombi ya manunuzi ya mazao ya msitu kijijini. Maombi yote lazima yaonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna au idadi ya miti mteja anategemea kuvuna.

b) Kamati ya Maliasili wakishirikiana na Halmashauri ya Kijiji watajadili na kupitisha ombi hilo endapo itaridhia kufuatana na matakwa ya mpango wa uvunaji.

c) Kijiji kitajibu maombi ya mnunuzi kwa maandishi kwa kutoa sababu za kumkubalia au kumkatalia mteja ombi lake. Muhtasari wa kikao cha kumjadili mnunuzi utaambatanishwa na majibu ya maombi yake.

d) Endapo maombi yatakubaliwa, Kibali cha uvunaji/ukusanyaji kitatolewa kikiwa na sahihi ya Mwenyekiti wa kamati ya maliasili na Mwenyekiti wa Kijiji pamoja na mihuri husika. Kibali kitaonyesha makadirio ya miti itakayovunwa na makadirio ya ujazo, pamoja na matawi.

e) Kabla ya kufanya manunuzi, muuzaji na mnunuzi wanatakiwa kuingia mkataba wa mauzo ya mazao ya msitu (Angalia fomu namba SF19).

f) Nakala tatu za kibali zitatolewa ambapo nakala moja itabaki kijijini , nakala halisi atabaki nayo mteja na nakala nyingine atapewa Afisa Misitu wa Wilaya (DFO). Nakala halisi pamoja na nakala ya Afisa Misitu wa Wilaya lazima zipelekwe kwa Afisa Misitu wa Wilaya kwa ajili ya uhakiki pamoja na nakala ya muhtasari wa kikao.

g) Nakala moja kati ya vibali viwili vilivyothibitishwa na Afisa Misitu wa Wilaya itatakiwa kutolewa nakala (kuburuzwa) na kurudishwa kijijini.

h) Kijiji kinatakiwa kutoa nakala ya ziada kwa Meneja wa Umoja wa Uthibitishaji ya kibali hicho, ingawa kiutendaji jukumu hili anaweza kulifanya mteja kwa niaba ya kijiji.

i) Mteja atawasiliana na Kamati ya Maliasili kwa ajili ya kuanza uvunaji rasmi.

j) Baada ya kupokea ujumbe wa kuanza uvunaji, Kamati ya Maliasili inatakiwa kubandika tangazo la uvunaji huu mapema kama inavyotakiwa na kipengele H8 cha Masharti ya Uanachama.

**S7.** Fomu *SF21 Uwiano wa Mauzo ya Magogo* inatakiwa kukamilishwa na kujazwa na meneja wa msitu baada ya kumaliza mauzo. Hii itatoa maelezo na kumbukumbu za utofauti uliojitokeza katka ujazo uliohitajika kuvunwa katika kibali, ujazo wa uvunaji halisi uliofanyika na ujazo uliouzwa wakati ukaguzi utakapofanyika. Maelezo mengine ya mapungufu yaliyojitokeza mfano, pia tarehe za uvunaji ulipofanyika kutofautiana na tarehe za uvunaji za kibali lazima maelezo yake yawekwe bayana katika fomu hii.

**S8.** Wanachama wa Umoja wa Uthibitishaji wanatakiwa kuwapa upendeleo zaidi wavunaji ambao ni wakazi au wakazi wa vijiji jirani ambao wako tayari kulipa gharama kiushindani kwa mazao ya msitu endapo tu upendeleo uliotolewa hautaathiri malengo yao ya kiuchumi. Mwanachama pia anaweza kufanya makubaliano ya kimkataba na wateja wa nje kwa miaka mingi endapo pande zote mbili zitapenda kufanya hivyo lakini wanatakiwa kutafuta soko la ndani kwanza na kumtaarifu Meneja wa Umoja wa Uthibitishaji.

## Hati ya Mauzo

**S9.** Mauzo yote lazima yawe na hati ya mauzo kwa kutumia kitabu cha *Hati ya Mauzo ya Mazao ya Msitu Yaliyothibitishwa* ambayo hutolewa na mwanachama wa umoja. Hati hizi lazima ziwe na jina la kijiji husika.

**S10.** Hati ya Mauzo ya mazao ya Msitu lazima iambatanishwe na maelezo ya kina ya mazao ya msitu yaliyovunwa kwa mauzo hayo mfano jamii ya miti iliyovunwa, ukubwa na vipimo vya kila gogo.

**S11.** Nakala nne za Hati ya mauzo zinatakiwa zikamilishwe na kusambazwa kama ifuatavyo:

a) Mnunuzi

b) Kumbukumbu za meneja wa Msitu

c) Ubao wa Matangazo wa kijiji (Tangazo hili likae kwa muda usiopungua wiki mbili)

d) Meneja wa Umoja wa Uthibitishaji

**S12.** Kila nakala ya Hati ya mauzo lazima isainiwe na Meneja wa Msitu na ipigwe muhuri.

**S13.** Hati ya mauzo isitumike kwa matumizi mengine tofauti na mauzo ya mazao ya msitu kutoka katika misitu ya kijiji iliyothibitishwa. Mwanachama wa umoja wa uthibitishaji hawatakiwi/hawaruhusiwi kuuza mazao ya msitu kutoka kwenye misitu ya nje ya msitu uliothibitishwa kama mazao yaliyothibitishwa.

## Ushauri wa Jumla juu ya Mauzo ya mazao ya Msitu

Ifuatayo ni orodha ya mapendekezo yatakayofanikisha mauzo ya mazao ya msitu kutoka kwenye Umoja wa Uthibitishaji Misitu na kuwaridhisha wanunuzi na wauzaji kwa pamoja na yameandaliwa kuhakikisha malengo yanaeleweka kwa kina kwa kila upande. Mapendekezo haya siyo ya lazima kufuatwa na mwanachama wa umoja wa uthibitishaji bali mwanachama anaweza kuona ni ya muhimu kwa lengo la kupunguza migongano/migogoro kati ya muuzaji na mnunuzi wakati wa kufanya mauzo ya mazao ya msitu. Pia yanalenga kudumisha mahusiano mazuri kati ya muuzaji na mnunuzi. Hata hivyo, mnunuzi na muuzaji wanatakiwa kukubaliana na wanaweza wasifuate mapendekezo haya ya nyongeza pale inapoonekana inafaa.

**S14.** Wauzaji pia wanaweza kuongeza gharama za huduma za ziada kwenye mkataba wa mauzo , mfano gharama za kumkodi msimamizi wa uvunaji . Hata hivyo wauzaji wanashauriwa kuweka makisio ya juu ya gharama za ziada kwenye mkataba kuepuka kuingia hasara, kwa mfano ikiwa haikuwa wazi ni siku ngapi msimamizi wa uvunaji atahitajika kusimamia zoezi hilo basi muuzaji aweke makisio ya juu ya siku za uvunaji.

**S15.** Wanunuzi wana haki ya kuuliza uwiano wa kiasi cha malipo ya awali wanachotakiwa kulipia kabla ya uvunaji, ila wauzaji wanatakiwa wajihadhari na kiasi cha madai hayo kwa sababu wanaweza kuwakosa wanunuzi wengine.

a) 50% ni madai ya busara kwa kila uvunaji mdogo ambao utamalizika mapema.

b) Mauzo makubwa na ukizingatia uvunaji utachukua muda mrefu, mnunuzi anaweza kutanguliza kiasi kidogo cha fedha kabla ya kuanza uvunaji, Mfano-uwiano kiasi cha 25%.

c) Ni busara kuomba 100% ya malipo ya awali kwa ajili ya huduma yoyote ya ziada ambayo muuzaji ameitoa kwa mnunuzi.

**S16.** Wauzaji wanatakiwa kutambua kuwa wateja/wanunuzi wanaotaka kununua mzigo mkubwa au wamejiandaa kununua mzigo mkubwa kwa miaka kadhaa mfululizo , wanaweza kupewa masharti nafuu kidogo ( Mfano, mahitaji ambayo yanalipiwa kwa kawaida yakaombwa kuwa bure). Kibiashara hili ni jambo la kawaida kufanyika na ni muhimu kuyapa kipaumbele maombi kama hayo. Hata hivyo wauzaji wanatakiwa kuwa makini kutofanya maamuzi yasiyo muhimu na watafute ushauri kutoka kwa Meneja wa Umoja wa Uthibitishaji iwapo maombi yatashinikizwa sana na mteja.

**S17.** Wauzaji wanatakiwa kuwa makini na kujua upekee wa mazao ambayo wanataka kuuza kwa kuzingatia kwamba wateja wanaweza kukosa mazao hayo sehemu nyingine, hata hivyo wauzaji wanatakiwa kutambua kuwa kwa kuweka gharama za juu sana wanunuzi wanaweza kuwachukulia kama wauzaji wasioweza kuaminika na hivyo kukataa kufanya biashara nao.

**S18.** Wateja/Wanunuzi au wawakilishi wao wanahitaji makabrasha ya aina tofauti ili waweze kusafirisha mzigo wao kutoka kijijini. Kwa kawaida makabrasha hayo ni pamoja na :

a) Nakala ya barua ya maombi ya kununua mzigo au Oda ya manunuzi (pale inapohitajika)

b) Kibali cha uvunaji kilichotolewa na Meneja wa Msitu.

c) Hati ya mauzo

d) Maelezo ya vipimo vya magogo yakiwa yameambatanishwa na hati ya mauzo

e) Kibali cha kusafirishia mzigo

f) Leseni ya biashara isiyopitwa na wakati (Kwa wanunuzi waliosajiliwa kama Kampuni)

**S19.** Wauzaji wanatakiwa kushirikiana na wanunuzi katika kukamilisha makabrasha ya maelezo kama yanavyoonekana hapo juu, hata hivyo ni jukumu la mteja au mwakilishi wake kuhakikisha kuwa makabrasha yao yote yako katika hali ya usahihi na kwa mpangilio maalumu kabla ya kuanza kusafirisha mazao hayo na makabrasha hayo yasiwe na mapungufu yoyote.

# Utunzaji wa Kumbukumbu

**F1.** Meneja wa Umoja pamoja na Wanachama wote wanatakiwa kutunza kumbukumbu zao zilizoainishwa hapo chini kwa kipindi cha kisichopungua miaka mitano.

### *Kumbukumbu za Wanachama*

**F2.** Wanachama wa Cheti cha pamoja cha uthibitishaji misitu ni lazima waweke kumbukumbu za usimamizi wa msitu wa jamii na kumbukumbu zingine za:

a) Mpango wa usimamizi msitu pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

b) Sheria ndogo zinazotumika pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

c) Maelezo yeyote ya tathmini ya rasilimali za misitu.

d) Mpango wa uvunaji ulioandaliwa kwa ajili ya msitu wa jamii.

e) Mihuitasari ya mikutano ya kamati za maliasili ni lazima itunzwe hata kama mikutano haukuhusu msitu uliothibitishwa ni vyema kumbukumbu zikawepo ili kuonyesha kuwa hakuna kumbukumbu yeyote ambayo haikutunzwa.

f) Kumbukumbu za kila doria.

g) Kila ziara iliyofanywa na MCDI na mpango wa urekebishaji uliotolewa.

h) Ziara zote zilizofanywa na watumishi wa serikali na mawsiliano yaliyopokelewa toka Serikalini kuhusiana na usimamizi wa msitu wa jamii.

i) Maombi yote ya kuvuna ndani ya msitu wa jamii au ya kuingia msituni kama ilivyobainishwa katika mpango wa usimamizi na hatua zilizochukuliwa dhidi ya maombi hayo.

**F3.** Wanachama pia lazima waweke kumbukumbu zote za fedha na matumizi yote yaliyofanyika kuhusiana na msitu wa jamii uliothibitishwa. Hii ni pamoja na:

a) Mapato yote yatokanayo na mazao ya misitu.

b) Mapato yote yatokanayo na faini na taarifa za uhalifu uliofanywa.

c) Matumizi yote yanayohusiana na shughuli za usimamizi msitu kama vile posho kwa wanadoria.

d) Faida iliyopatikana, kwa mfano faida iliyotolewa na kamati ya maliasili kwa serikali ya kijiji.

**F4.** Kumbukumbu zote ni lazima zionyeshe taarifa zifuatazo inapobidi;

a) Tarehe.

b) Mahudhirio ya mikutano ya kamati na doria.

c) Rasilimali za misitu, jamii za miti na kiasi.

d) Mlipaji (jina la kampuni).

e) Mapato.

**F5.** Taarifa za fedha za Mameneja wa Misitu ni Lazima zikaguliwe wakati wa zoezi la ukaguzi la mwaka. Kama kuna mapungufu yanayozidi asilimia 10% ya kipato au matumi, Mwongozo wa Urekebishaji Utatolewa.

**F6.** Taarifa zote zilizoelezwa hapo juu ni lazima zitunzwe kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.